

MFUMO WA USAJILI WA VIZAZI NA VIFO

Hii ni huduma mpya inayomuwezesha muombaji kujaza Fomu ya Maombi ya cheti cha kuzaliwa au kifo kwa njia ya Kielektroniki akiwa mahali popote. Baada ya kujaza fomu ya maombi ya cheti cha kuzaliwa au kifo, atatakiwa kuichapisha (Print) na kuiwasilisha pamoja na vielelezo vingine katika Ofisi ya Wilaya iliyo karibu naye kwa ajili ya kushughulikiwa maombi yake ya Cheti.

VIELELEZO VINAVYOHITAJIKA WAKATI WA UJAZAJI WA FOMU YA MAOMBI YA CHETI CHA KUZALIWA.

1. Tangazo la kizazi kwa vizazi vilivyosajiliwa ndani ya muda katika vituo vya tiba
2. Kadi ya Kliniki
3. Cheti cha ubatizo
4. Pasi ya kusafiria
5. Cheti cha kumaliza elimu ya msingi au secondari (leaving certificate)
6. Kitambulisho cha Utaifa au Kadi ya kupigia kura
7. Vitambulisho vya Utaifa au Kadi ya kupigia kura vya wazazi
8. Picha ya Mwombaji ya hivi karibuni yenye kivuli cha rangi ya buluu isiyokoza (Light blue Background)

Zingatia/Muhimu

Mwombaji lazima aambatishe vielelezo si chini ya viwili kati ya hivyo vilivyotajwa pamoja na vitambulisho vya wazazi.

VIELELEZO VINAVYOHITAJIKA WAKATI WA UJAZAJI WA FOMU YA MAOMBI YA CHETI CHA KIFO

1. Tangazo la kifo kwa kifo kilichoandikishwa ndani ya muda katika kituo cha tiba

Kwa kifo kilichotokea nyumbani au kuchelewa kuandikishwa mwombaji aambatishe

- **BARUA YA UTAMBULISHO:** Mwombaji wa cheti cha kifo kilichochelewa kuandikishwa anatakiwa kuleta barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kata/kijiji wa eneo tukio lilipotokea. Barua hiyo inatakiwa itaje majina kamili ya marehemu, tarehe ya kifo, mahali alipofia na sababu za kifo. Vilevile picha ndogo ya Mwombaji iweke kwenye barua hiyo na igongwe muhuri.
- **MUHTASARI WA KIKAO CHA WANANDUGU:** Ndugu wa marehemu wanatakiwa wakae kikao na kuandaa muhtasari ambao una agenda za kikao ambazo pamoja na mambo mengine ni kumteua msimamizi wa mirathi ambaye ndiye atakayetambulika kisheria kufuatilia cheti cha kifo. Kikao kihudhuriwe na ndugu wa marehemu. Pia watatakiwa kuorodhesha majina yao na kuonyesha uhusiano wao na marehemu. Ndugu hao

watatakiwa waweke sahihi kuthibitisha ushiriki wao. Muhtasari huu uthibitishwe na Afisa Mtendaji wa Kata/kijiji kwa kugonwa muhuri na kuweka sahihi yake.

ANGALIZO: Ifahamike kuwa muhtasari huo unatakiwa ushirikishe ndugu wote wa karibu wa marehemu ili kuondoa migogoro inayoweza kutokea. Pia endapo Msajili atakuwa na mashaka juu ya yaliyomo katika muhtasari huo anaweza kuwaita baadhi ya waliohudhuria kwa mahojiano zaidi.

- HATI YA KIAPO: Hati ya kiapo kutoka mahakamani au kwa mwanasheria iliyoapiwa na mwombaji (Msimamizi wa Mirathi) na kueleza taarifa za marehemu kama majina kamili, tarehe ya kifo na mahali alipofia na sababu za kifo

Uhakiki wa Vyeti vya Vizazi na Vifo

Hii ni huduma mpya inayomuwezesha muombaji kuwasilisha maombi ya kuhakiki cheti cha kuzaliwa na kifo kwa njia ya Kielektroniki akiwa mahali popote. Muombaji atatakiwa kuscan cheti cha kuzaliwa au kifo anachohitaji kihakikiwe na kisha kukituma kwa njia ya kielektroniki ili kihakikiwe. Majibu ya uhakiki yatatumwa katika akaunti uliyofungua sehemu iliyoandikwa **“View Status”**

Linki ya kuingia katika mfumo: <https://online.rita.go.tz>